

Mitazamo ya Kusawiri Wahusika wa Kike katika Tamthilia za Kiswahili: *Posa za Bikisiwa na Mama Ee*

John Mutua*, Rocha Chimerah, Nancy Ngowa

Department of Languages, Linguistics and Literature,

Pwani University, PO Box 195-80108, Pwani Kenya

Email: mutua660@yahoo.com

* Corresponding author

Received: April 14, 2017

Published: May 17, 2017

Ikisiri

Uhusiano kati ya jinsia ya kiume na ya kikeni ni suala linaloendelea kuzua mijadala si haba mionganoni mwa jamii kila uchao. Aghalabu midahalo hiyo huibua mitazamo kinzani baina ya wasomi na wahakiki wa kazi za kifasihi. Baadhi ya kazi hizo za kifasihi ni zile zilizohakikiwa kwa misingi ya nadharia ya kifeministi. Tahakiki hizo zimekuwa zikichochea fikira kwamba, waandishi wa kiume ndio wanaopaswa kulaumiwa kwa kuendeleza usawiri usiopendeza kwa wahusika wa kike katika fasihi. Hali hii imevyaza dhana kuwa waandishi wa kiume huwasawiri wahusika wa kike kwa mtazamo tofauti wakilinganishwa na waandishi wa kike. Ikiwa mawazo hayo ni ya kusadikika, basi itakuwa sawa na kudai ya kwamba waandishi wa kike huwasawiri wahusika wa kike kwa mtazamo unaopendeza katika fasihi. Je, waandishi wa kiume husawiri wahusika tofauti na waandishi wa kike? Ili kulijibu swali hili tumelinganisha waandishi wa jinsia tofauti. Kufungamana na mkabala huu wa uwazaji, makala hii imelinganisha waandishi wa jinsia ya kike na ya kiume kwa lengo la kubainisha mitazamo yao kuhusu usawiri wa mhusika wa kike katika tamthilia za Kiswahili. Tumelinganisha tamthilia ya mwandishi wa kike; *Mama Ee* ya Mwachoffi A. (1987) na *Posa za Bikisiwa* (2003) ya waandishi wa kiume amba ni; King'ei K. na Mohamed S. Tamthilia ya *Posa za Bikisiwa* ilichapishwa miongo miwili baada ya *Mama Ee* na hivyo inadhihirisha mtazamo tofauti wa taswira ya kike ikilinganishwa na *Mama Ee*. Hata hivyo, mpito wa wakati huenda umechangia mabadiliko katika mitazamo ya kusawiri wahusika wa kike. Pia, inakisiwa kuwa jinsia ya mwandishi inaathiri usawiri huu. Waandishi wa tamthilia hizi waliwapa wahusika wa kike sifa mbalimbali ambazo zinaashiria mitazamo yao. Licha ya kwamba waandishi hao wote wamejadili maudhui sawa, wameonyesha tofauti ya kimtazamo katika masuala ya uongozi, utabaka, ndoa na upotovu wa kimaadili mionganoni mwa maudhui mengine. Ili kufikia lengo la makala hii tumeongozwa na nadharia ya ufeministi wa Baada-ukoloni. Nadharia hii imetuwezesha kuchunguza sifa za mwanamke Mwfrika kama alivyosawiriwa na waandishi wa Kiafrika.

Istilahi Muhimu

Chanya – Inayopendeza, -enye thamani, -enye kustahili au kinyume cha hasi.

Mtazamo – Namna kitu, jambo au hali inavyofikiriwa kuwa, hisia alizonazo mtu kuhusu mtu, kitu au hali.

Mwanamke – imetumika kurejelea wanawake (wingi).

Ufeministi wa Baada-ukoloni – Nadharia ya uhakiki wa fasihi inayohusishwa na mtazamo wa Kiafrika.

@ 2016 by the author(s); Mara Research Journals (Nairobi, Kenya)

1. UTANGULIZI

Usawiri wa wahusika hutegemea kwa kiwango kikubwa ubunifu wa mwandishi. Jambo hili pia hutokana na sifa za binadamu walio katika jumuiya yake anaotaka wawakilishwe na wahusika hao. Sifa za wahusika

hao aghalabu hufichua mitazamo ya msanii anayehusika kumhusu mhusika fulani. Wahusika huteuliwa kimafumbo kwa kusudi la kujiepusha na shari itokanayo na kuwazungumzia au kuwakejeli baadhi ya watu binafsi katika jamii ya mwandishi. Hali hii yamkini ndiyo aliyohofia mwandishi wa riwaya ya *Shamba la Wanyama* George Orwell (tafsiri ya 1967) alipowateua wahusika wengi wanyama. Mfano wa huu unalenga kuonyesha kuwa wahusika wa fasihi wanaweza kuwa viumbwe wa kila aina; wawe wanyama, ndege, mazimwi, malaika, wadudu, miungu, viumbwe visivyo hai na hata binadamu. Wahusika wasio binadamu huhusishwa sana na utanzu wa hadithi za fasihi simulizi, Wamitila (2003). Tamthilia nyingi za kissasa huwatumia wahusika binadamu. Wahusika hao huwa wa kiume na wa kike. Pamekuwepo na mdahalo unaoendelea mionganoni mwa wahakiki wa kazi za fasihi unaobia madai kwamba waandishi wa jinsia tofauti huwasawiri wahusika wao wa kike kwa mitazamo tofauti. Tahakiki nyingi za tamthilia za Kiswahili zinazopatikana katika maktaba ya vyuo vikuu vimelipigia darubini suala la usawiri wa wahusika wa kike. Baadhi ya watalaamu ambao wamehusisha usawiri hasi wa wahusika wa kike na waandishi wa kiume ni pamoja na Wamitila (2003), Mbatiah (2000) na, Chesaina (1987). Mathalani, Chesaina alipokuwa akitathmini jinsi watunzi wa tamthilia wa Kiafrika walivyomsawiri mhusika wa kike katika kazi zao, alihakiki tamthilia mbili za Penina Muhandi Mlama, *Hatia* (1972) na *Nguzo Mama* (1972). Alionyesha kuwa wanaume hawana uwezo wa kuzungumzia utata wa maisha ya mhusika wa kike vilivyo kiuchumi au kijamii. Mule (1991) aliunga mkono maoni ya Chesaina ya kwamba mwanamke ana nafasi bora katika kulitalii suala la usawiri wa mwanamke katika fasihi kuliko mwanamume.

Basi, ikiwa mawazo ya wataalamu hawa ni ya kutegemewa, mwanafasihi hanabudi kujiuliza; je, ni kweli kuwa waandishi wa kike huwasawiri wahusika wa kike kwa mtazamo chanya (unaopendeza) katika kazi zao za kifashi? Halikadhalika, ni kweli kuwa waandishi wa kiume kwa upande wao huwasawiri wahusika wa kike kwa mtazamo hasi (usiopendeza). Maswali haya ndiyo tuliyoshughulikia katika makala hii. Ili kuyajibu tumechunguza usawiri wa mhusika wa kike katika tamthilia za Kiswahili za waandishi wa jinsia mbili. Mwandishi wa kike ni Ari Katini Mwachof, *Mama Ee* (1997) na Said A. Mohamed na Kitula King'ei, *Posa za Bikisiwa*. Tamthilia hizi ziliandikwa katika karne tofauti; *Mama Ee*, karne ya ishirini na *Posa za Bikisiwa* karne ya ishirini na moja. Kama ilivyo ada kwa sanaa yoyote, fasihi haina budi kuakisi mabadiliko yanayoshuhudiwa katika jamuiya ya mwandishi ili ikubalike na wasomaji. Mabadiliko tunayokusudia katika makala hii ni yale yanayohusu usawiri wa mwanamke. Kadri mitazamo ya jamii kuhusu nafasi ya mwanamke inavyoendelea kubadilika, ndivyo athari ya mabadiliko hayo inavyozidi kuhisiwa katika sanaa za kifashi. Katika makala hii tumeonyesha jinsi mabadiliko ya mitazamo ya kijamii yalivywakumba wasanii wa utanzu wa tamthilia ya Kiswahili.

2. MABADILIKO YA USAWIRI WA MWANAMKE KATIKA FASIHI

Taswira ya mwanamke anayokumbana nayo msomaji Katika *Mama Ee* ni ile yenyenye mtazamo wa kihafidhina ambao umekuwepo tangu jadi kama wanavyodai wahakiki wa tanzu za fasihi. Mtaalamu Ndungo, (1998) katika tasnifu yake akilinganisha taswira ya mwanamke katika vitendawili vya jamii ya Agikuyu (Wakikuyu) na ya Waswahili aligundua taswira duni ya mwanamke katika jamii hizo mbili. Sifa za mwanamke kwa mujibu wa utafiti wake ni; kutoaminika, kutotegemewa na mtegemezi. Uchunguzi wake ulifichua mtazamo hasi kwa wahusika wa kike wanaotajwa katika vitandawili vya jamii ya Wakikuyu na Waswahili. Ingawa uchunguzi wake ulijikita katika fasihi simulizi ulidhihirisha mitazamo iliyokuwemo katika jumuiya yake wakati huo. Taswira hiyo yamkini ndiyo iliyowachochea waandishi wa tamthilia za Kiswahili za wakati huo kuwasawiri wahusika wa kike katika mtazamo hasi. Uchambuzi wa tamthilia ya *Mama Ee* unadhihirisha mawazo kama hayo.

Utafiti wa Ndungo (1988) na Momanyi (1998) unahusiana kwa kuwa zote zilichunguza taswira ya mwanamke ingawa katika ushairi. Momanyi aliyahakiki mashairi ya Muyaka Bin Hajji, Utendi wa Mwanakupona na ushairi wa Shaaban Robert Kulingana naye, taswira duni ya mwanamke iliendelea kutawala katika kipindi chote baina ya miaka (1840 - 1960) takriban muda ambao mashairi hayo yaliandikwa. Aliendelea kueleza kuwa washairi ambao waliandika miaka hiyo ni pamoja na Mwanakupona

(1860), Muyaka Bin Hajji (1840) na Sheikh Shaaban Robert (1960). Taswira hii inaonekana ilikuwepo karne nyingi zilizopita ijapokuwa hatuwezi kusema kuwa hapakuwepo na dalili za mabadiliko ya mitazamo ambayo labda yalisababishwa na vuguvugu na mihemko ya kutetea haki za wanawake mionganii mwa jamii iliyozuka mara kwa mara kabla ya kudhibitiwa na hisia za kitamaduni na kidini. Baadaye katika mashairi ya Sheikh Shaaban taswira ya mwanamke ilionekana kubadilika kadiri wakati alioandika ulivyozidi kubadilika, kulingana na Momanyi (1998) ‘Mabadiliko yaliyotokea katika jamii yalimfanya Shaaban Robert kutupilia mbali imani ya kidini na ya kihafidhina’. Imani hiyo ya kihafidhina inashukiwa kuwa ndiyo inayomchochea kumsawiri mwanamke katika mashairi yake ya awali kama kiumbe laghai, asiyeaminika wala kutegemewa. Sifa hizo zinampa Shaaban Robert aonekane msanii mwenye mtazamo hasi kuhusu usawiri wa wahusika wa kike katika mashairi yake ya awali. Hata hivyo, mtazamo huu wake ulibadilika baadaye kutokana na kile Momanyi anachokiona kama kuathiriwa na mabadiliko ya kiuchumi na maendeleo ya kijamii katika mfumo wa kibepari. Yamkini mtazamo wa Shaaban Robert ulibadilika baada ya kushuhudia wafanyakazi wakidai haki zao na hata kuamrisha vyama vyta kisiasa nchini Tanganyika kama vile Chama Cha Waafrika na TANU ili kumwondoa mkoloni. Aliweza kushuhudia wanawake wakidai haki zao pia. Yaelekea mazingira haya ndiyo yaliyomchochea kumsawiri mwanamke kinyume na itikadi yake ya awali ya kihafidhina iliyochangiwa na imani yake katika dini ya Kiislamu.

Mabadiliko ya mtazamo wa Shaaban Robert kuhusiana na usawiri wa mwanamke yanawiana na yale yanayowasilishwa na Ali Mazrui katika tamthilia ya *Kilio cha Haki* ambayo iliandikwa (1982) takribani miongo miwili baada ya mashairi ya Shaaban Robert kuandikwa. Ingawa nia ya makala hii si kulinganisha mashairi ya kale na tamthilia za kisasa wala mtazamo wa watafiti wa fasihi simulizi na mtazamo wa wasanii wa karne ya ishirini na moja tunafanya hivyo kwa kusudi la kusisitiza jinsi matukio na mitazamo ya jamii inavyoathiri taswira ya mwanamke inayoakisiwa katika fasihi ya Kiswahili.

Katika miaka ya hivi karibuni, waandishi wa tamthilia za Kiswahili wanaonekana kufufua mitazamo chanya kwa mhusika wa kike ambayo mara kwa mara imekuwa ikizuka na kufifia mionganii mwa jamii. Hali hii ndiyo inayoshuhudiwa katika *Posa za Bikisiwa*, tamthilia iliyoandikwa katika karne ya ishirini na moja. Yamkini waandishi wa tamthilia hii wameathiriwa na mawazo ya jamii ya Wakenya walimokulia na kuandikia. Mtazamo wao kuhusu wanawake unadhibitishwa na kuhidhinishwa kwa katiba ya taifa la Kenya mwaka wa 2010. Katiba hiyo inahimiza Wakenya kuwapa wanawake thuluthi moja ya nafasi katika bunge la taifa na seneti kama nyezo ya kuhakikisha usawa wa kijinsia katika taifa. Hata hivyo, uhakiki wa tamthilia zilizoandikwa na waandishi wanawake hazielekei kuafiki mawazo hayo. Mfano mwema ni *Dunia Hadaa* (2007) ya Catherine Kisovi ambayo ina mtazamo sawa na *Mama Ee* (1987) ya Katini Mwachofi ijapokuwa kazi hizo ziliandikwa katika vipindi tofauti.

3. USAWIRI WA MWANAMKE KATIKA MAMA EE

Taswira ya mwanamke inayoshuhudiwa katika *Mama Ee* inawakilisha mtazamo wa mwandishi ambao ni mwigo wa jamii kuhusu nafasi ya mwanamke wakati huo. Mathalani, kupitia usawiri wa viongozi wa Chama cha Umoja wa Wanawake unaozungumziwa na Mwavita na nduguye Tenge, uongozi wa wanawake unatiliwa shaka. Wanawake viongozi wanaotarajiwa kuwakilisha na kuonyesha juhudhi za kujaribu kusuluuhisha baadhi ya matatizo ya wenzao pasipo ajizi wala ubaguzi. Katika dondo hili Mwavita anaigiza nafasi na wakuu wa chama:

TENGE: Mwisho niliuliza je, kugandamizwa kina mama na hawa wanaume? Sheria mbaya ya talaka?
Kina mama vijijini? Watumwa vijijini?

MWAVITA: (Akiwaiga wakuu wa chama) “Sisi hatukuja hapa kuzungumza juu ya talaka. Hatutaki kuvunja maisha ya kijamia. Tumalize mkutano, bwanangu karibu atakuja nichukua! (Ha! ha! ha! Wote wacheka)

TENGE: Ndiyo maana Mwavita akasema hakuna umoja wa kina mama! Ni umoja wa nini Mwavita?

MWAVITA: Wa watumwa! (uk.94)

Wakuu wa chama cha Umoja wa Wanawake hawataki kujishughulisha na madhila yaliyowasakama wanawake wenzao wanaoishi vijiji ambapo idadi kubwa ya wanawake huishi. Pia, hawakuwasadia Tenge na Mwavita walipokuwa na tatizo linalohusu ndoa. Walisema si shughuli yao kuijingiza katika mambo ya familia. Aidha, hawataki kushiriki katika kuzirekebisha sheria mbovu zinazochangia kudhulumiwa kwao, badala yake wamehiari kuliachia jukumu hilo mawakili wanaojua sheria.

TENGE: Kweli siongezi lolote. Mke mnene! Baada ya kumweleza yote yaliyotokea kesini na mpango wetu wa kuungana na kina mama wote kupinga sheria mbaya ya jamaa alisema huku akipiga miayo na kupigana na usingizi (amwiga)“Sisi chama chetu si chama cha sheria. Hatuwezi kupigana na mahakama. Sheria hatuzielewi. Tuwaachie wanasheria wetu wapiganie na kurekebisha zilizo mbaya!”

MWAVITA: Mmeshangaa! Kweli ndivyo alivyosema mkuu huyo... uk.94

Ni kinaya kuwa chama hiki kimeundwa kwa lengo la kuyatatua baadhi ya matatizo ya wanawake. Kando na lengo hili chama hicho cha wanawake kinaendeleza udhalimu dhidi yao na wala hakina uwezo wa kutatua kadhia yoyote. Kwa hivyo, msomaji anahisi kuwa baadhi ya matatizo ambayo wanawake wanadai kupata yanachangiwa na wenzao. Mwandishi anadhihirisha mtazamo hasi kwa kutuchorea taswira ya wanawake wanaoendeleza uadui dhidi ya wenzao.

Mtazamo huo halikadhalika unaendelezwa kuitia sifa ya ubaguzi inayodhihirishwa na viongozi wa muungano huo wa wanawake. Muungano huo ni wa akina mama wote lakini umejengwa na wanawake wa tabaka la juu na kuwabagua wale wa tabaka la chini, wasio na elimu na wanaoishi mashambani. Viongozi wao huletwu ofisini kwa magari makubwamakubwa. Hawayashughulikii matatizo yanayowahusu kina mama wanaoishi vijiji. Wanadinda kuyajibu maswali ya Tenge na Mwavita wakidai yanahuus maswala ya familia na chama chao hakiyashughulikii hayo. Chama hicho, “Umoja wa Kina Mama” hakipo kwani viongozi wake wanawaenzi wanaume na ni cha wanawake wasomi na wa tabaka la juu, hawajui taabu za kina mama vijiji. Sifa ya kubaguna wao kwa wao inawachora wahusika wanawake kwa mtazamo hasi.

TENGE: Ungekuwako ungefikiri nchi hii hakuna kina mama maskini. Nilishangaa. Maana asilimia tisini ya kina mama hapa nchini wako vijiji, wengine hata hawajaingia garini.

MWAVITA: Walipoanza kuzungumza ndipo tulipojua kuwa hicho chama ni cha kina mama waliosoma na walio na walio katika tabaka la juu. Hawajui kabisa taabu za kina mama vijiji, kutembea maili kumi kutafuta maji; wao walikuwa wakizungumza juu ya vitanda vibovu katika hospitali ya kuzalia kina mama hapa mjini na wakunga wajeuri! Kijiji je? Hakuna hospitali, hakuna wakunga licha ya wakunga wajeuri? (uk.94)

Tabia ya maafisa wa chama hicho la kuwapuuza Tenge na Mwavita inadhihirisha jinsi wanawake matajiri na wasomi wanavyowadharau wanawake wa tabaka la chini. Kwa hakika huu ni ubaguzi kwa sababu masuala wanayopendelea ni yale yasiyohusu masilahi ya kila mmoja kama vile uhaba wa vitanda na wakunga wajeuri katika hospitali za umma. Hilo halielekei kuwa tatizo la kila mwanamke. Jambo hili linaonyesha kuwa wanawake viongozi na walio na hali bora kiuchumi huwabagua wale wa ngazi za chini

kiuchumi na hasa wanaoishi mashambani. Wahusika wa kike wamesawiria kama wanaobaguana wao kwa wao. Hii ni taswira hasi kwa wahusika wa kike.

Ari Mwachofi anatuchorea taswira nyingine ya wanawake wengi makahaba. Mwavita anamshutumu mumewe kwa kutumia pesa zake kwa mahahara wa vilabini. Kinaya anakasirishwa na shutuma hiyo na akamuuliza mkewe kama kulikuwa na makahaba waliomzidi Tenge ambaye ni dadaye Mwavita. Taswira hii ni inasisitiza mtazamo wa mwandishi kuhusu wahusika wa kike.

MWAVITA: “..Huku pesa zote zaishia kwa mahawara na togwa. Juma huyo angeambulia patupu kama si pesa zangu. Tena wataka kuniachia kazi. Nikae hapa nawe ufuatane na wake zako...

KINAYA (*Asimama na kumnyoshea kidole*) Wewe fyata domo lako chafu. Mahawara! Kuna mahawara mji huu zaidi ya dadako Tenge! Ati mwanafunzi! Bila shaka nawe ungekuwa kama yeye ningekawiya kidogo kukuowa. Shukuru nilikuowa mapema. Nausiponiheshimu mimi nyumbani kwangu utatoka ufuate uhawara na hayo meno yang'oke tuone utaishi wapi. Shika adabu yako unaposema na mimi unasilika?

MWAVITA: (*Amesonga mbali*) Wewe ulinioa nilipokuwa mwana-mwali sasa ushanifanya mama waniita hawara! Aah! Kinaya ndugu yangu! Wanidharau hivyo?

KINAYA: Tenge dadako si hawara? Siku zote “George ananipeleka cinema-twende ngomani”. Ngoma hiyo tutaiona mwisho wake. (uk.7)

MWAVITA: Ukitaja ya Tenge wanilazimu kukueleza ya dada zako. Dada zako wote watatu wako wapi? Wazurura ovyo mjini kama mbwa koko bila mabw... (uk.7-8)

Mwandishi amewasawiri wanawake wengi kama wanaorandaranda mijini huku wakiwanyakua mabwana za wenzao na kulewa na kushiriki ukahaba. Wanawake hao wanasawiriwa kama wanaopenda anasa na kuwdhulumu mabibi kwa kushiriki na mabwana zao ulevi na umalaya. Wengine wanakwenda ngomani na cinema. Hii ni taswira hasi kwa wahusika wa kike.

Katika hali nyingine mwandishi huropa wahusika wengine wanaotagusana na yule anayemzungumzia lugha ya kumtambulisha. Lugha inayotumiwa na mhusika kumtambulisha mhusika mwensiwe inaweza kuashiria jinsi mwandishi angependa wasomaji wamfasiri mhusika mlengwa. Mfano mwema ni ule wa Baba Tenge na Kakake wanapomshutumu Tenge kwa vitendo vyake visivyowapendeza. Wote wawili wanapewa mtazamo wa kumdhililisha mwanamke huyo.

Baba Tenge anatumia lugha ya kudhalilisha dhidi ya bintiye. Baba anamwita bintiye Malaya. Maneno haya yanadhalilisha hasa yikitoka kinywani cha babamtu yakielekezwu kwa bintiye kama inavyodhihirika hapa.

BABA: Pesa zangu zote za darasa la kwanza hadi sasa nazitaka; sijali utazipata vipi hata kama ni kwa kuongeza uhawara. (*Akimgeukia mkewe na kumsukuma*) na wewe walilia nini? Hivi ndivyo unavyowalea wasichana wako?

BABA: Wacha nimfundishe Malaya huyu apate kuregesha pesa zangu zote nilizopoteza ati karo ya shule, kumbe ni karo ya kujifunza umalaya (uk. 12).

Ni kweli kuwa Tenge amewakosea wazazi wake kwa kupata mimba na kufukuzwa shulen. Wazazi wake wamehuzunishwa na kukasirishwa na kitendo chake. Hata hivyo, Tenge naye ameonyesha ukaidi kwa kutotii maaso ya mamake na nduguye Mwavita na sasa matokeo ni kuhimili mimba haramu na kutumia vibaya pesa za wazazi wake. Baba anamwadhibu kwa kumpiga. Hata hivyo, lugha anayotumia babake kwa

kumshutumu bintiye mkosa inaonyesha ukosefu wa tasfida. Kwa baba kumwita bintiye malaya ni maneno makali tukitilia maanani uhusiano wa mtu na mwanawewe. Baba akiwa mzazi anatarajiwa awe na maneno yanayomstahili mzazi kwa mwanawewe hata kama kitendo alichokifanya bintiye kinachukiza. Makosa ya mtoto hayamwondolei mtoto huyo haki ya kuheshimiwa na babake. Aidha, mwandishi anaendeleza mawazo ya kitamaduni (Kiafrika) anapompa mhusika mwanamume, yaani Baba Tenge kumlaumu mkewe kwa makosa ya binti yao kana kwamba makosa ya mwana (wa kike) ni ya mamake na wala si babake. Kwa hivyo, mhakiki anadadisi lugha ambayo mwandishi amempa mhusika huyo ili kueleza uchungu aliokuwa nao juu ya tabia ya mwanawewe. Msomaji anahisi kuwa huo ni udhalilishaji na usawiri hasi wa mtoto wa kike. Kakake pia anamwita Tenge hawara licha ya kwamba yeye pia ni mmoja wao kwani amewapachika mimba wasichana wengi. Vilevile, aliyekuwa rafiki yake shulenii, George anamwita hawara pasipo kuzingatia yale waliyoyafanya walipokuwa marafiki. Huu ni udhalilishaji wa wahusika wa kike na ni dhihirisho la mtazamo hasi wa mwandishi kuhusu wanawake.

Mara nyingi mwandishi amemsawiri Mwavita kama mwanamke mjeuri. Taswira hii huenda ni kinyume na azima yake kudhihirisha namna anavyoteswa na mumewe. Ingawa msomaji anamwonea huruma Mwavita na kuchukizwa na vitendo vya Kinaya vya kumdhulumu mkewe. Pia ni muhimu kutambua kuwa kauli ya mumewe Kinaya anapokabiliwa na wazee wakimtaka awaeleze sababu za kumpiga mkewe, analalamika kuwa mkewe huchochea hasira zake kwa ujeuri wake. Mwavita alimtukana mumewe mara kwa mara. Taswira inayojengewa msomaji ni ya mwanamke mtukutu na mjeuri.

MWAVITA: Tangu jana huoni mimi naumwa! Usiku kucha sina mtu wa kunipa maji. Usingizi sina kwa kuumwa na kwa wasiwasi tele juu yako. Wafika saa hizi wataka mkeo avae nguo ukajionyeshe naye katika tafrija! Sitaki. Waona una ua hapa? “Nenda zako uso kama ubao huna haya! (uk. 49)

Wahenga walisema maneno matamu humtoa nyoka pangoni. Hatuoni Mwavita akitumia unyenyekevu ili kusuluuhisha ugomvi wake na mumewe. Kiafrika aghalabu mwanamke anatarajiwa awe na lugha ya upole hata wakati wa kutolewana baina yake na mumewe. Pengine yaliyomfika Mwavita aliyachochea mwenyewe kupitia lugha aliyoitumia kwa mumewe. Kinaya anathibitisha haya anapoulizwa kujitetea dhidi ya mashtaka yaliyomkabili mbele ya wazee. Alisema haya:

MZEE WA KIJIJI: Kinaya una lolote la kusema juu ya haya yote yaliyosemwa juu yako?
Lazima ujitetee.

KINAYA: “...pia Mwavita alikuwa mjeuri sana kwangu. ...Ndiye aliyenitia wazimu wa kumpiga. ...”
(uk. 35)

Mwandishi anasisitiza kuwa wanawake hawa waliteswa kutokana na ujeuri wao na wala si ukatili wa waume zao. Anaelekea kushadidia mtazamo wake kuwa madhila mengi yanayowakumba wanawake yana chanzo chake kwa wanawake wenyewe. Hayo ndiyo mwandishi huyu anayoelekea kusisitiza katika onyesho la tatu la sehemu ya pili.

TENGE: Ndiyo maana Mwavita akasema hakuna umoja wa kina mama! Ni umoja wa nini Mwavita?

MWAVITA: Wa watumwa!

TENGE: Ehe ndio hasa, wote walikuwa watumwa wametekwa na pesa, wanaume, anasa...

MWAVITI: Na pia ujinga, kutojua. Hawajui lolote linalotendeka nje ya jamii yao ndogo ya watumwa.Yale yanayohusu asili mia tisini ya kina mama hawayajui wala hawajali kuchunguza, hawana haja kabisa kujua. Uk.95

Kauli hii imebainisha wazi mtazamo wa mwandishi wa kike kuhusu wahusika wanawake.Huu ni mtazamo hasi kwa wahusika wa kike.

4. USAWIRI WA MWANAMKE KATIKA POSA ZA BIKISIWA

Suala la uongozi wa mwanamke limejitokeza tena katika tamthilia ya Said Ahamed Mohamed na Geofrey Kitula King'ei.Waandishi hawa wanaelekea kuupa usawiri wa mwanamke sura mpya.Mtazamo huu ni chanya ukilinganishwa na wa Ari Mwachofi katika *Mama Ee* ambao ulielekea kumsawiri mhusika wa kike kama aliyeshindwa na majukumu ya uongozi hasa unaowanufaisha wenzake.Kinyume na maoni ya Mwachofi, waandishi wa *Posa za Bikisiwa* wanamsawiri mwanamke kama kiongozi anayependwa na kuteuliwa na wengi kutokana na weledi na ushupavu wake.Sifa ya mwanamke kiongozi inadhihirika kupitia mhusika mkuu Bikisiwa.

Mfalme ambaye ni babake Bikisiwa anatambua kuwa, sio jambo rahisi kumdhhibit mwanamke wa kisasa ambaye anasoma mengi na kutagusana na malimwengu na ulimwengu wa nje. Anagundua kuwa ni muhimu kutupilia mbali tamaduni zinazowataka wazazi kuwachagulia binti zao wachumba. Mfalme anamruhusu bintiye kufanya maamuzi kuhusu suala hilo. Baada ya raia kushuhudia jinsi Bikisiwa anavyoishia kukabiliana na sinikizo zilizohusu ndoa yake na kuibuka mshindi, wanataka awe kiongozi wao. Wote wanamkulali kama kiongozi wao ambaye wanamtarajia kuleta mabadiliko ya desturi kuhusu nafasi yao.Mwandishi anasema kuwa wanaume wameshindwa na uongozi na kuwapisha wanawake.

WOTE:(Huku wakimzunguka na kumkumbatia Bikisiwa) Tunakulinda ukitulinda Bikisiwa.Tumeshauona uongozi wako wa kike.Viongozi wa kiume wameshindwa.Tuna hamu na wewe. Tumeshauona uongozi wako wa kike.Viongozi wa kiume wameshindwa. Tuna hamu na wewe.Tuna hamu na kiongozi wa kike mwenye ukweli kama wewe.Kiongozi wa kike mwenye hisia na utu halisi.Kiongozi wa kike mwenye kujali wake na waume. (uk.68)

Mwandishi ameonyesha kushindwa kwa wanaume uongozini, hafanyi hivyo ili kuonyesha wanaume si viongozi bali anataka kusisitiza kuwa hata wanawake wanaweza kuwa viongozi wema.Sifa za kiongozi mwema zimetambuliwa.Anapaswa awe mkweli, mwenye utu na afanyaye usawa kwa watu wa jinsia zote.

SAUTI: (Baada ya ukwenzi mkali...) Wananchi wako tayari Bikisiwa. Wako tayari kabisa! Wanangojea viongozi wao shupavu tu. Kike kwa kiume tuko tayari Bikisiwa, tunangojea viongozi wetu shupavu... (uk.75)

Mwandishi ameonyesha kukubalika kwa Bikisiwa kuwa kiongozi na raia wote kama kulikochochewa naye kumiliki sifa zote zinazomwafiki kiongozi mwema. Mtazamo chanya wa mwandishi kuhusu wanawake unadhihirika wazi hapa.

Waandishi wa *Posa za Bikisiwa* wamemsawiri mwanamke anayekataa kuruhusu mwili wake kutumiwa na wanaume kwa maslahi yao au kushirikishwa katika ukahaba ama hata ndoa isiyo na mwafaka mwema ili kupata zawadi au mamlaka.Kupitia kwa waposaji mbalimbali wanaomtaka urafiki Bikisiwa, anasawiriwa kama mwanamke anyepinga kunyanyaswa.Chachi ni mmoja wa waposaji anayetumia mbinu za kijanja ili avutie mapenzi ya Bikisiwa.Chachi anapousifu uzuri wa Bikisiwa kama njia ya kumpumbaza kwa sifa teletele, Bikisiwa anautambua ujanja wake na kumkemea kwa ukali.Katika kauli yake anajidhihirisha kama mtu asiyekubali kuchezewa mwili wake na anayejali haki zake kama mwanamke. Mwandishi anaelekea kumsawiri kwa namna hii ili kudhihirisha mtazamo wake kwa wahusika wa kike.

BIKISIWA: (Anamkatisha) Basi tu! Umekuwa wimbo wenu nyinyi nyote. Mnadhani thamani ya mwanamke ni umbo! Mara nywele, mara shingo, mara madodo, sijui kiuno... Mimi ni mtu bwana. Ninastahili heshima kamili. Ninahitaji kutazamwa kama mtu siyo kitu cha kuchezea. (uk.49)

Katika dondoo hili Bikisiwa anasawiriwa kama anayetetea hadhi na thamani yake kama mwanamke. Anapinga kutumiwa visivyo na wanaume huku wakimpa sifa za kumpumbaza. Anajitetea. Mwandishi anadhihirisha mtazamo chanya kwa mhusika wa kike.

Katika suala la ndoa, waandishi hao pia wamemsawiri mwanamke mwenye msimamo dhabiti katika lengo lake. Bikisiwa ameposwa na watu wengi. Baadhi yao ni matajiri, mashujaa na wana wa wafalme. Wote wamejaribu kumshawishi kwa kumpa zawadi chungu nzima. Kuna waliompa vitabu, mapambo, mavazi na tunu nyinezo za thamani kubwa. Hayo yote hayakudiriki kuushawishi wala kuulainisha moyo wa Bikisiwa. Hulka hii yake ya kutoghibiwa na sifa na zawadi anazopewa ni ishara ya kuwa na msimamo dhabiti kinyume na jinsi wanawake wanavyodhaniwa kuwa. Anajasiri kumwambia Hassan kenyekenyé kuwa hamtaki.

BIKISIWA: "... Unaweza kulowea, ukaoa atakayekupenda akakupenda na kuzaa naye, lakini huwezi kunioa mimi kwa sababu moja kubwa. Mimi sitaki kuolewa na wewe. Mimi sikupendi. (uk.32)

Bikisiwa anaonyesha msimamo usiotetereka anaposema kuwa hata akiozwa kwa lazima katu hatampa atakayekuwa mumewe moyo wake. Ujasiri huu unamshtua Hassan. Malkia pia anasisitiza hali hii ya kutotawaliwa na ukale. Anabainisha wazi kuititia kwa kitabu anachosoma kiitwacho "Nitaoleta nikipenda" kuwa yeche kama alivyo bintiye hawako tayari kuiendeleza desturi ya kale ya kutafutiwa wachumba.

Waandishi wa *Posa za Bikisiwa* anaendelea kubainisha mtazamo wao kwa usawiri wa wanawake kama wahusika waliozinduka kuhusu nafasi yao katika jamii. Katika kifunguzi, mwandishi anatuchorea taswira ya mwanamke aliyezinduka na kuazimia kuwashamasisha watu wengine juu ya maovu wanayofanyiwa wanawake katika ndoa kote ulimwenguni.

MWANAMKE: "Wewe! Au husikii? (Anamwonyesha kidole mtu mmoja ndani ya hadhira) zibua masikio yako uzingatie. Hii ni tamthilia ya hasara na hasira. Jiulize kwa nini miaka, mikaka na karne zote hizi wametuandama sisi?" hawataki hata tupoe hata kidogo (uk.1).

Dondoo hili linaonyesha mwamko mpya alionao mwanamke na vilevile chuki aliyonayo dhidi ya wanawake wenzake ambao wameshindwa kutambua jinsi wamekuwa wakidhulimiwa miaka nenda miaka rudi katika taasisi ya ndoa. Pia waandishi wanaendelea kutuchorea taswira ya mwanamke aliyetambua na ambaye hawezu kudanganyika kuhusu ndoa njema. Katika dondoo hili mwanamke ameonyesha kuzinduka katika suala la ndoa na pia anawahamasisha wengine wazinduke.

MWANAMKE: "...(*Anageuka nyuma*) Nyinyi mnaochuchumaa nyuma. Nani nyinyi enh, mnaotaka kujichoma katika ndoa isiyojadiliwa? (*Sasa anasema kwa sauti ya juu na nguvu zaidi*) Si vibaya kuposana iwapo posa ni yenye nia njema. Si vibaya kuoana iwapo ndoa ni ya kuheshimiana (uk.2)

Mwanamke anaendelea kulalamika na kipinga vikali nia ya wale wanaomtaka usuhuba bila kujali hisia zake. Anapinga njama za kijanja za baadhi ya waposaji wanaotumia hila kumshirikisha katika ndoa isiyo na mafanikio. Katika utongoaji wake mwanamke analitupa kando fugu alilokuwa amejifunika nalo usoni. Kitendo hiki kinaweza kufasiriwa kama kufungua macho, kuamka au kuzinduka kutoka katika giza la kutofahamu haki zake katika ndoa.

MWANAMKE: Niko tayari kuposwa

Lakini lazima muwaonye waposaji:
 Nguvu hazifai
 Enyi mnaojitia uume mjinga kesha tambua
 Nguvu zenu hazifai! (uk.5)

Anatambua kuwa ni haki yake kuposwa na waposaji wanaojali maslahi yake na ambao hawatumii mabavu dhidi yake. Mtazamo huu wa wanawake ni tofauti na wa mwanamke wa zamani ambaye alichaguliwa mchumba na wazazi na akamkubali bila maswali. Msimamo huu unafichua taswira ya mwanamke aliyezinduka na mweledi wa mambo. Huu ni usawiri chanya kwa mhusika wa kike na unaodhahirisha mtazamo wa mwandishi kuhusu wanawake.

Mazungumzo baina ya binti mfalme, Malkia na Mfalme yanadhirisha kuwa wanawake ni wasomi wa wapekuzi wa mambo mbalimbali. Hii ni kuonyesha kuwa wanatangamana na maarifa na mawazo mengi kuhusu nafasi yao katika jamii yao. Vilevile, hujifunza mengi kuhusu uhusiano wao na wanaume katika ndoa. Wamegundua kupitia somasoma zao kuwa dini na ndoa ni asasi zinazotumiwa na jamii kuwakandamiza.

BIKISIWA: Aaah Mama! Si juzi mbichi tu nimekuona ukisoma tamthilia iitwayo ‘Nitaoleta Nipendelea’ iliyoandikwa na Ngugi Wa Thong’o? Je, Umeshaimaliza?

MALKIA: “... Tuliisoma kwa mkupuo mmoja bila ya kusita tokea mwanzo hadi mwisho. Ama kweli, kumbe dini na ndoa huweza kutumiwa na malaghai kubatilisha mambo na kuwaadhibisha watu wasio na hatia?” (uk.17)

Wanawake wote katika tamthilia hii wanapinga ukandamizwaji unaoendelezwa na jamii kwa misingi ya kudumisha tamaduni. Kinyume chake wameazimia kufuata ndoto zao za maisha bila kushurutishwa na wanaume au kusalimu amri kutokana na vitiisho vinavyowakabili katika jamii.

Anatambua kuwa maisha ya ndoa hayategemei mali au hadhi ya mtu bali ni maelewano na maridhiano baina ya mume na mke. Yeye anaweka wazi msimamo wake kuwa hatafuti majagina bali anataka mume mwenye asili ya kwao na atakayemwoa bila masharti yasiyofaa au yanayopendelea upande mmoja.

BIKISIWA: (anasimama na kumshika bega babake na kwenda naye mbele ya hadhira, halafu anatongoa kishairi) Baba. Naomba ufanye kulihali
 Unipunguzie idhilali
 Hapa hebu nipe dalili
 Posa zipigwe darubini kali
 Iwe posa njia mbili
 Tuposane kwa adili
 Jumuiko la wawili
 Lenye tija, heshima na mustakabali... (uk.23)

Mwandishi anamsawiri Bikisiwa kama aliyezinduka kutoka katika lepe la usingizi wa kutojua haki zake.

Waandishi hao wanaendelea kumsawiri mwanamke kama aliye mastari wa mbele sio tu kutetea hali yake bali ya taifa lake. Cecilia na Jane walikuwa mionganoni mwa waandamanaji waliokuwa wakitetea haki zao. Ingawa malalamiko yao si dhahiri katika maandamano haya, ni wazi kuwa Jane na Cecilia walitoroka kwao wakiogopa udhalimu wa aina nyingi. Hatua yao kukimbilia mjini ili kuepuka kabakwa na kuozwa kwa watu matajiri ni dhihirisho kuwa hawakudiriki kuwaruhusu hata jamaa zao waingilie haki zao. Kama

anavyodai Mpitanja katika fujo hizo walipigwa marungu, risasi zenye marisao ya mipira na chuma na mabomu ya kutoa machozi. Wanawake waliotambua dhuluma wanayofanyiwa katika jamii wanaandamana. Wanavumilia mateso ya askari na hawafi moyo. Huu ni ujasiri unaovyazwa hamu ya kutetea haki zao.

MTAMBAJI: Watu wanapodai haki zao, hiyo haiitwi fujo. Ni shinikizo la kimyakimya kudai haki zao. (uk.41)

CECILIA: Wengi lakini katika maandamano yale walikuwa wanawake. Huu kwa mujibu wao utakuwa ukurasa mpya wa fujo. (uk.42)

Juhudi nyingine za kutetea haki zao zinadhihirika katika makabiliano ya maneno baina ya Bikisiwa na Chachi. Chachi anapousifu uzuri wa Bikisiwa kama njia ya kumpumbaza kwa sifa teletele, Bikisiwa anautambua ujanja wake na kumkemea kwa ukali. Kwenye maneno yake anajidhihirisha kama mtu mwenye msimamo dhabitи na anayejali haki zake kama mwanamke. Mwandishi anaelekea kumsawiri kwa namna hii ili kudhihirisha mtazamo wake kwa wahusika wa kike.

5. HITIMISHO

Kutokana na tathmini ya tamthilia hizi mbili, ni wazi kuwa mwanamke ameweza kupitia mabadiliko makubwa. Mabadiliko haya hayakutokea siku moja. Yamekuwa yakindeka kadiri ya wakati. Jambo hili limeweza kushughulikiwa katika tamthilia za kisasa kama vile *Posa za Bikisiwa*. Zaidi ni kuwa waandishi wa kiume kama vile Mohamed na King'ei wameweza kubainisha mabadiliko haya katika uandishi wao. Kuimarika kwa nafasi ya mwanamke kiasi cha kubainika na mwanamume ina maana kuwa kwa hakika yamekuwa mabadiliko makubwa.

Awali uongozi wa mwanamke ulikuwa wa kutiliwa shaka. Huu ni uongozi unaosawiriwa na Mwachofi katika *Mama Ee*. Wahusika Mwavita na Tenge wanaeleza kuwa viongozi wa chama cha wanawake hawakubainisha wala kushughulikia matatizo ya wanawake wote kama ilivyotarajiwa. Matokeo yake ni kushindwa kwa chama hiki kutekeleza dhima yake. Kilikuwa kimeundwa kwa nia ya kutatua matatizo yote yaliyomkabili mwanamke. Hakishughulikii tatizo lolote. Upande mwengine, mwanamke wa kisasa katika *Posa za Bikisiwa* amepevuka kiasi cha kuwa kiongozi bora, bora hata kuliko mwanamume. Bikisiwa ana sifa zote bora ambazo kiongozi hutarajiwa kuwa nazo. Hii ndio maana anakubali na kukubaliwa kuwa kiongozi wa raia wote.

Mwanamke wa awali katika *Mama Ee* alikuwa mbaguzi katika misingi ya utabaka. Walio matajiri walikuwa wanawadharau na kuwapuuza wa tabaka la chini. Kando na kuwa matajiri, wanawake wa tabaka la juu ndio waliosoma. Wake wa matajiri wanawadharau maskini kama vile Tenge na Mwavita. Wanapounda chama chao, kinakuwa ni cha kutetea maslahi ya tabaka la juu peke yake. Hali ni tofauti katika *Posa za Bikisiwa*. Mwanamke anatetea hadhi yake kama mwanamke bila ubaguzi. Hawajiangalii kwa misingi ya kitabaka bali wanajali maslahi ya wote.

Kwa mujibu wa mwandishi wa *Mama Ee*, mwanamke amesawiriwa kama kahaba. Mwanamke anayejiruhusu kutumiwa na mwanamume kujinufaisha na kujifurahisha bila kujali hisia zake binafsi na aila yake. Hawa ni kama vile Tenge na Mwavita. Japo hali hii inapigwa chuku, ukweli ni kuwa mwanamke huyu alitumiwa sana na mwanamume. Tenge anatiwa mimba angali mwanafunzi. Jambo hili linamfedhehi na kuifadhaisha jamaa yake. Mwanamke katika *Posa za Bikisiwa* anakataa kabisa mwili wake kutumiwa vibaya na mwanamume. Hataki kuingizwa katika ndoa asiokuwa na usemi kama mwenzake mwanamume.

Katika *Mama Ee* sawa na *Posa za Bikisiwa* mwanamke ni jeuri. Akiunga mkono kauli hii, Wafula (2012) anahojji kuwa mabadiliko yanapotokea, hayabadiishi kila kitu. Baadhi ya vipengele vya awali huweza

kujitokeza katika usasa baada ya mabadiliko kutokea. Hivyo, Ujeuri wa mwanamke aliyesawiriwa na Mwachofi haukubadilika. Unajitokeza tena katika usawiri wa King'ei na Mohamed. Katika sawiri zote hizi, mwanamke hanyenyekie kwa mwanamume namna inavyotarajiwa katika tamaduni za Kiafrika. Mwavita haonekani kunyenyekiea kwa mumewe kama njia ya kusuluhisha mgogoro uliokuwapo baina yao. Anamkabili ana kwa ana. Naye Bikisiwa anadai kuwa hata akiozwa kwa lazima, hatakubali kumpa mume huyo moyo wake kama hamtaki.

Waandishi wa tamthilia zote mbili vilevile wanaonekana kupatana kuwa ndoa na dini ni vipengele ambavyo hutumiwa na mwanamume kumkandamiza mwanamke. Hata hivyo, katika usawiri wa Mwachofi mwanamke ameathirika sana na masuala haya. Usawiri nao wa King'ei na Mohamed unaonyesha mwanamke akijaribu sana kukwepa dhuluma za aina hizi. Mwanamke hapa amezinduka na kubainisha chanzo cha dhuluma yote inayomkumba.

6. MAREJELEO

- George O. (1967) *Samba la Wanyama*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.
- Kisovi, N. (2007) *Dunia Hadaa*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foudation.
- Kenya constitution, (2010) "Representation of the people". Nairobi: Government Printer.
- Mwachofi, A. (1987) *Mama Ee*. Nairobi: Heinemann.
- Mazrui, A. na Njogu, K. (2006) *Sudana*. Nairobi: Longhorn Publishers (K) Ltd.
- Mazrui, A. (1987) *Kilio cha Haki*. Nairobi: Longhorn
- Mbatiah, M. (2001) *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing.
- Mohamed, S. na King'ei, K. (2008) *Posa za Bikisiwa*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Ndungo, C. (1985) 'Wanawake na Mabadiliko ya Kihistoria Katika Kiswahili'. Tasnifu ya M.A: Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).
- Ntarangwi, M. (2004) *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Augustana College, Rock Island, IL 61201.
- Wamitila, K. (2002) Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele Vyake. Nairobi: PhoenixmPublishers Ltd.
- (2003) *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.
- Wafula, R. (1999) *Uhakiki wa Tamthilia: Historia na Maendeleo Yake*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.
- Wafula, R. Na Njogu, K. (2007) *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.
- Wamitila, K. (2003) Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Cite this article:

Mutua, J., Chimerah, R. and, Ngowa, N. (2017). Mitazamo ya Kusawiri Wahusika wa Kike katika Tamthilia za Kiswahili: *Posa za Bikisiwa na Mama Ee*. *Mara res. j. Kiswahili*, Vol. 2, No. 1, Pages 1 - 11, ISSN 2520-0577